

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA KILIMO

Anuani ya Simu "Ushirika"  
Simu: +255 26- 23 22456  
Telefax: +255 26- 23 21973  
B. Pepe:  
[ushirika@ushirika.go.tz](mailto:ushirika@ushirika.go.tz)



Tume ya Maendeleo ya Ushirika  
Mtaa wa 'Kuu',  
S. L. P 201,  
**DODOMA**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. LA.93/288/01/37**

**03 Mei, 2019**

Wenyeviti na Wajumbe

Bodi za Vyama vya Ushirika vya Ufuta, Soya, Choroko, Dengu na Mbaazi,  
**RUVUMA, SHINYANGA, MWANZA, LINDI, PWANI NA MANYARA.**

**Yah : WARAKA WA MRAJIS NA. 1 WA MWAKA 2019 KUHUSU  
MAELEKEZO YA SERIKALI YA UENDESHWAJI NA USIMAMIZI WA  
BIASHARA YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, SOYA NA MBAAZI  
MSIMU WA 2019/2020 KUPITIA MFUMO WA VYAMA VYA USHIRIKA**

### 1.0. UTANGULIZI

- 1.1. Serikali kuitia Wizara ya Kilimo ilitoa maelekezo juu ya mfumo mpya wa uendeshwaji wa biashara ya mazao ya wakulima kuitia Vyama vya Ushirika kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. **Katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Ruvuma, Lindi, Pwani na Manyara na Halmashauri zake ndizo zinazohusika na Mfumo huu wa Vyama vya Ushirika kwa kuanzia na kadiri ya muda unavyoruhusu, huduma hii itakwenda katika maeneo mengine.** Hii ni kutokana na kuweka mpango mzuri wa usimamizi na udhibiti upande wa **Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.** Lengo la Serikali la kuweka mfumo huo mpya wa kiuendeshaji, ni kutaka kuhakikisha kuwa, kilimo cha zao la **Dengu, Choroko, Ufuta, Soya na Mbaazi** kinamnufaisha mkulima sanjari na kuondoa mfumo holela wa ununuzi wa mazao hayo ambayo kimsingi ulikuwa haumnufaishi mkulima.

1.2. Aidha, kwa kuzingatia dhamira hiyo pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Serikali, na mamlaka ya Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuitia Sheria ya Vyama Vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake; Tume ya Maendeleo ya Ushirika inatoa maelekezo maalum kwa **Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika vya zao la Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi katika maeneo yaliyoainishwa** juu ya uendeshwaji na usimamizi wa biashara ya zao la **Ufuta, Soya na MBAazi** hususan katika msimu wa 2019/2020 kwa hatua za utekelezaji.

## **2.0. UTARATIBU WA UENDESHWAJI NA USIMAMIZI WA BIASHARA YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, SOYA NA MBAAZI KWA MSIMU WA 2019/2020 KUPITIA VYAMA VYA USHIRIKA**

Bila ya kuathiri matakwa ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika NA.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015 pamoja na Sheria zingine husika, utaratibu wa ukusanyaji na uuzwaji wa zao la **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** ya mkulima kuitia Ushirika utazingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Kila mkulima mwenye zao la **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kwa ajili ya kuuza atatakiwa kupeleka katika ghala la Chama cha Msingi akiwa amehakiki kiwango cha ubora kwenye madaraja yanayotambulika kwa mujibu wa Sheria na kanuni za zao husika;
- (ii) Chama cha Ushirika cha Msingi kitatakiwa kuhakikisha kabla ya msimu wa ukusanyaji wa mazao hayo kuanza, mzani unaotumika kupimia utakaguliwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) chini ya sheria ya vipimo na mizani hapa nchini;
- (iii) Chama cha Ushirika cha Msingi kitatakiwa kupokea **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kutoka kwa wakulima, kitatakiwa kuzihifadhi katika magunia/mifuko mipyä (PP Bags) yenye viwango vya ubora vilivyothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS);
- (iv) Chama cha Ushirika cha Msingi kitatakiwa kuhakikisha kuwa uzito halisi wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** ni kilo 50 kwa kila mfuko/gunia kabla ya kupeleka kwenye ghala la mnada;

- (v) Chama cha Ushirika cha Msingi kitatakiwa kuandika jina la chama chake na namba ya utambulisho iliyotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kila Mfuko/gunia la Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi kwa kutumia mfano ufuatavyo:-

**CROP: .....**

**SEASON: 2019/2020**

**ORIGIN: Tz**

**SOURCE: SONAMCU/01- (*Nambari Chama hudumiwa na SONAMCU LTD;***

- (vi) Chama cha Ushirika cha Msingi kitatakiwa kupeleka **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** za wakulima wake kwenye ghala la mnada lililosajiliwa na lililo karibu yake kwa ajili ya mauzo;
- (vii) Chama cha Msingi kitatakiwa kusafirisha **Ufuta, Soya, Dengu, Choroko na MBAazi** za wakulima kwenda ghala kuu la mnada kwa kutumia Produce Delivery Note (PDN) ya Chama cha Ushirika cha Msingi ikiambatana na **fomu ya orodha ya wakulima iliyojazwa kikamilifu** ya wamiliki wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** husika ikiwa katika nakala nne; nakala ya kwanza ipelekwe kwa Afisa Ushirika,nakala ya pili Chama Kikuu husika, nakala ya tatu Msimamizi wa ghala husika, na nakala ya nne ibaki katika Chama cha Msingi chenyewe;
- (viii) Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika wa Halmashauri husika watatakiwa kukokotoa gharama ya kusafirisha mazao husika kwa kuzingatia umbali halisi kati ya Chama cha Ushirika cha Msingi husika na ghala la mnada;
- (ix) Chama cha Msingi kitapaswa kuhifadhi na kutunza ubora wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kwa kuzingatia madaraja na kanuni za ubora kama zitakavyoainishwa na mamlaka husika.

### **3.0. WAJIBU NA MAJUKUMU YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA KUSIMAMIA UENDESHWAJI WA BIASHARA YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, SOYA NA MBAAZI MSIMU WA 2019/2020**

#### **3.1 Wajibu na Majukumu ya Vyama Vikuu vya Ushirika katika kusimamia biashara ya Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi.**

Pamoja na mambo mengine, Wajibu na Majukumu ya Vyama Vikuu vya Ushirika (UNION) katika kusimamia uendeshwaji wa biashara ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** msimu wa 2019/2020 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuandaa na kusambaza shajala kwa ajili ya ununuzi katika Vyama Vya Msingi;
- (ii) Kuhamasisha wakulima wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** kuijunga katika AMCOS;
- (iii) Kusimamia shughuli za uendeshwaji wa biashara ya zao la **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** kuititia AMCOS;
- (iv) Kusimamia malipo ya fedha za mauzo ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** ya Mkulima na kuweka utaratibu rafiki wa malipo kwa wakulima husika kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika wa Wilaya husika pamoja na Viongozi na Menejimenti za AMCOS husika;
- (v) Kuweka utaratibu wa kampuni za ununuzi wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** kulipa gharama ya ununuzi wa zao kwa Vyama Vya Msingi na Vyama Vikuu kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika pamoja na wadau wengine wa usimamizi katika Halmashauri ya Wilaya husika;
- (vi) Kuhamasisha AMCOS kufungua Akaunti benki zitakazotumiwa na Wanunuzi kulipia fedha za gharama za ununuzi wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi**;
- (vii) Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na Mbaazi** kutoka kwa Wakulima na kutoa taarifa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) pamoja na wadau wengine wa usimamizi pindi zinapohitajika;
- (viii) Kusimamia na kutekeleza majukumu mengine ya msingi kwa kadiri yatakavyokuwa yakitolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

**3.2 Wajibu na Majukumu ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) katika kusimamia uendeshwaji wa biashara ya Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi msimu wa 2019/2020.**

Pamoja na mambo mengine, Wajibu na Majukumu ya Vyama vya Ushirika vya Msingi katika kusimamia uendeshwaji wa biashara ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** msimu wa 2019/2020 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuajiri Watendaji waadilifu, waaminifu na wenyewe uzoefu na biashara ya zao la **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi**;
- (ii) Kufanya usafi wa Maghala ya kuhifadhi **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** chini ya uratibu na usimamizi wa mamlaka husika;
- (iii) Kufukiza dawa (fumigation) kwenye Ghala zote zitakazotumika kwenye ukusanyaji wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi**;
- (iv) Kupokea na kuhifadhi kwa usalama wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** iliyowasilishwa chamani kabla ya kuisafirisha kwenda kwenye Ghala Kuu husika;
- (v) Kuhakiki ubora na uzito wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kabla ya kupokea.
- (vi) Kutoa nyaraka sahihi za mapokezi ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi**;
- (vii) Kuandaa orodha ya malipo kwa wakulima (payment schedule) kwa malipo stahiki ya wakulima wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kwa kufuata mtiririko wa mapokezi ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi**;
- (viii) Kusimamia malipo ya wakulima;
- (ix) Kusimamia uendeshwaji wa biashara ya zao la **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kwa kushirikiana na wadau wa Usimamizi;
- (x) Kuhamasisha wakulima wasiokuwa wanachama kuijunga na AMCOS;
- (xi) Kutunza kwa usahihi takwimu mbalimbali za ukusanyaji na malipo kwa wakulima;
- (xii) Kusimamia malipo ya makato/tozo mbalimbali za kisheria;
- (xiii) Kuhamasisha wanachama na wakulima kufungua Akaunti za Benki kwa ajili ya Malipo ya mauzo;

(xiv) Kusimamia na kutekeleza majukumu mengine ya msingi kadiri yatakavyokuwa yakijitokeza kwa kushirikiana na wadau wengine wa usimamizi.

#### **4 UTARATIBU WA MGAWANYO WA GHARAMA ZA UENDESHAJI WA BIASHARA YA ZAO LA DENGU, CHOROKO, UFUTA, SOYA NA MBAAZI**

Kwa mujibu wa Waraka huu pamoja na Sheria zingine husika, kila mnunuzi wa **Dengu, Choroko, Ufuta, Soya na MBAazi** atalazimika kulipa bei si chini ya bei elekezi ya msimu husika. Bei hii itaweza kubadilika kadiri ya Maelekezo kutoka kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Ushirika.

#### **5. MFUMO WA MALIPO YA FEDHA ZA MAUZO YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, SOYA NA MBAAZI KWA WAKULIMA KATIKA MSIMU WA 2019/2020**

Mfumo wa malipo ya fedha za mauzo ya **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kwa msimu wa 2019/2020 utakuwa ni utaratibu wa wakulima kulipwa fedha taslimu kuitia katika Vyama vya Ushirika vya Msingi. Aidha, kwa Vyama ambavyo vitatumia utaratibu wa malipo kuitia kwenye Akaunti za Wakulima husika, malipo hayo yanatakiwa kufanyika kwa wakulima **ndani ya siku mbili (2) za kazi** tokea siku ambayo **Dengu, Choroko, Ufuta, Soya na MBAazi** ilinunuliwa na kulipiwa kwenye AMCOS husika.

#### **6. UFUNGAJI WA VITABU NA UANDAAJI WA HESABU, UANDAAJI WA RASIMU YA TAARIFA ZA FEDHA, MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA, PEMBEJEZO NA VIFUNGASHIO PAMOJA NA MAKADIRIO YA BAJETI YA MAENDELEO**

Baada ya msimu wa **Dengu, Choroko Ufuta, Soya na MBAazi** kukamilika, kila Chama cha Ushirika kitapaswa kufunga vitabu vya hesabu, kuandaa rasimu ya taarifa za fedha, makisio ya mapato na matumizi ya kawaida, pembejezo na vifungashio pamoja na makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa kutumia **Mwongozo** utakaotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania na kutakiwa kuwasilisha nyaraka hizo kwa Mrajis au Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika kwa hatua za mapitio, uchambuzi, ushauri na uidhinishwaji.

## 5 HITIMISHO

Utekelezaji wa Waraka huu unahitaji usimamizi wa karibu wa **Maafisa Ushirika** pamoja **Mrajis Msaidizi** wa Vyama vya Ushirika Mkoa katika eneo husika. Aidha, utekelezwaji wa matakwa ya Waraka huu pia utaambatana sambamba na uzingatiwaji wa matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2015 na Sheria nyingine za nchi na **Miongozo mbalimbali inayotolewa na Wadau wa Usimamizi** (Ofisi ya Mkuu wa mkoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vyama vikuu vya ushirika, Vyama vya ushirika vya msingi, Wakulima, Wanununuzi/wafanyabiashara, Wakala wa vipimo, Taasisi za fedha, Wasafirishaji, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ya Ghala, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Taasisi ya Soko la Bidhaa (TMX), Waendesha Maghala, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Bandari, Wasindikaji wa Dengu, Choroko, Ufuta, Soya na MBAazi, Benki Kuu ya Tanzania (**BOT**), Kamati za Ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya).

## 6 Nawatakieni utekelezaji mwema.



Tito B. Haule

### KAIMU MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

**Nakala:** Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 980,  
**DODOMA.**

“ Mhe. Japhet Hasunga (Mb),  
Waziri wa Kilimo,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**40487 DODOMA.**

- “ Mhe. Joseph Kakunda (Mb)  
Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji,  
S.L.P. 2996,  
**DODOMA.**
- “ Mhe. Innocent Bashungwa (Mb),  
Naibu Waziri wa Kilimo,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**40487 DODOMA.**
- “ Katibu Mkuu,  
Wizara ya Kilimo,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**40487 DODOMA.**
- “ Mkurugenzi Mtendaji,  
Bodi ya Usimamizi Stakabadhi za Ghala,  
S.L.P. 38093,  
**DAR ES SALAAM.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P. 310,  
**MANYARA.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.1054,  
**LINDI.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.320,  
**SHINYANGA.**
- “ Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.320,  
**SHINYANGA.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.119,  
**MWANZA.**

- “ Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.119,  
**MWANZA.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.3080,  
**PWANI.**
- “ Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.74,  
**RUVUMA.**
- “ Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P. 74,  
**RUVUMA.**
- “ Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.  
**PWANI.**
- “ Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.  
**MANYARA.**
- “ Wakuu wa Wilaya,  
**Wilaya zinazolima Ufuta, Soya na MBAAZI,**  
**RUVUMA NA MANYARA.**
- “ Wakurugenzi Watendaji,  
Halmashauri za Wilaya,  
**Wilaya zinazolima Ufuta, Soya na MBAAZI,**  
**RUVUMA, SHINYANGA, MWANZA, LINDI, PWANI, NA**  
**MANYARA.**

- “ Mkurugenzi Mkuu,  
Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB),  
**DODOMA.**
- “ Mtendaji Mkuu,  
Soko la Bidhaa (TMX),  
S.L.P. 31632,  
**DAR ES SALAAM.**
- “ Kaimu Mkurugenzi Mkuu,  
COASCO,  
S.L.P 761,  
**DODOMA.**
- “ Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika (M),  
**MIKOYA RUVUMA, SHINYANGA, MWANZA, LINDI,**  
**PWANI NA MANYARA.** - *(Kwa hatua za usimamizi na Uratibu)*
- “ Maafisa Ushirika wote katika maeneo husika,  
**TANZANIA BARA.** - *(Kwa hatua za usimamizi)*
- “ Watendaji Wakuu wa Vyama Vya Upili na Kati,  
**TANZANIA BARA.** - *(Kwa hatua za utekelezaji na usimamizi)*
- “ Kaimu Katibu Mtendaji,  
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),  
S.L.P 2567,  
**DAR ES SALAAM.** - *(Kwa taarifa)*